# NOTISI YA PAMOJA YA DESTURI ZA FARAGHA

## NOTISI HII INAELEZA JINSI TAARIFA ZA MATIBABU KUKUHUSU ZINAVYOWEZA KUTUMIWA NA KUFICHULIWA NA JINSI UNAYVYOWEZA KUZIFIKIA TAARIFA HIZI—TAFADHALI IKAGUE KWA UANGALIFU.

Notisi hii inatumika kama notisi ya pamoja kwa hospitali, vituo na watoa huduma wanaoshirikiana na BJC Health na Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington (kwa pamoja zikijulikana kama "sisi" au "yetu" au "sisi") ya desturi za faragha zinazohusiana na taarifa za afya. Tumeanzisha mpango mmoja au zaidi ya huduma za afya zenye mpangilio. Sio vituo vyetu vyote vinavyoshiriki katika mpangilio huu wa pamoja wa huduma za afya. Hospitali na watoa huduma wote wanaoshirikiana na BJC Health hushiriki haswa katika mpangilio mmoja wa pamoja wa huduma za afya; katika mpangilio mwingine wa pamoja wa huduma za afya sehemu ya hospitali na watoa huduma waliounganishwa na BJC Health hushirikiana na Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington. Hii inamaanisha kwamba taarifa zako za afya zinaweza kushirikiwa kati ya washiriki katika kila moja ya mipango hii kwa madhumuni yanayohusiana na kushirikiana kwao kama mifumo ya afya iliyojumuishwa, ikiwa ni pamoja na utoaji wa tiba, kwa madhumuni ya malipo na kwa uwanda mpana wa shughuli za huduma za afya, ambazo zinaweza kujumuisha ukaguzi wa pamoja wa matumizi, utoaji hati, elimu, udhibiti wa hatari, usalama wa wagonjwa, tathmini ya ubora na shughuli za uboreshaji. Taarifa za ziada zinaweza kupatikana katika sera za BJC Health kuhusu mipango ya huduma za afya zenye mpangilio, zinazopatikana kwenye BJC.org/patients-visitors/our-policies.

Tutafuata masharti ya Notisi hii tunaposhiriki au kufichua taarifa zako za afya na kila mmoja na wahusika wengine. Kwa sababu tunahifadhi taarifa za afya kwa njia tofauti, tutajibu maswali, maombi na malalamishi yako kwa njia tofauti kuhusu taarifa zako za afya.

## MAJUKUMU YETU KUHUSU TAARIFA ZAKO ZA AFYA

Tunahitajika kisheria kulinda faragha ya taarifa zako za afya zinazolindwa, kukupa notisi ya majukumu haya ya kisheria na kukuarifu kutokana na ukiukaji wa taarifa za afya zinazolindwa ambazo hazina ulinzi. Notisi hii inaeleza jinsi, wakati na sababu tunatumia na kufichua taarifa za afya na haki zako za faragha kuhusu taarifa zako za afya. Katika Notisi yetu, tunaita matumizi na mifichuo yetu ya taarifa za afya kama "Desturi za Faragha." Taarifa za afya zinazolindwa kwa kawaida zinajumuisha taarifa tunazounda au kupokea zinazokutambulisha wewe na hali yako ya afya ya zamani, ya sasa, au ya baadaye, au huduma ulizopokea au malipo ya huduma hiyo ya afya. Tuna wajibu wa kutii Desturi hizi za Faragha kuanzia tarehe iliyoandikwa hapa chini.

## ATAKAYEFUATA NOTISI HII

Notisi yetu inatumika kama Notisi ya Pamoja na tutafuata masharti ya Notisi hii. Notisi hii inaeleza Desturi za Faragha za BJC Health na kampuni zake tanzu na vituo shirika inavyomiliki kikamilifu na watumishi ("maeneo shirika ya BJC") walioelezwa katika orodha iliyo kwenye BJC.org/patients-visitors/patient-privacy, na Desturi za Faragha za Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington na kampuni zake tanzu na vituo shirika inavyomiliki kikamilifu na watumishi. "Watumishi" ni pamoja na wataalamu wa afya, waajiriwa na watu wanaojitolea wa shirika na kituo chochote kulingana na Notisi hii.

## MABADILIKO KWENYE NOTISI HII

Tuna haki ya kubadilisha Desturi za Faragha na masharti yetu ya Notisi hii. Ikiwa tutafanya mabadiliko kwenye Notisi hii, tutakupa Notisi iliyosahihishwa kwa kuwezesha uipate kwa kutuma ombi na kwa kuichapisha kwenye maeneo yetu ya huduma. Pia tutachapisha Notisi iliyosahihishwa kwenye tovuti zetu. Mabadiliko yoyote tunayofanya kwenye Desturi zetu za Faragha yataathiri taarifa yoyote ya afya inayolindwa tunayohifadhi.

## JINSI TUNAVYOWEZA KUTUMIA NA KUFICHUA TAARIFA ZA AFYA KUKUHUSU BILA RIDHAA WALA IDHINI YAKO YA MAANDISHI

### Kwa Tiba, Malipo na Shughuli za Huduma za Afya

• **Kwa Tiba Yako** Tunaweza kutumia na/au kufichua taarifa zako za afya kwa watoa huduma wa afya na watumishi wengine wanaohusika katika huduma yako na ambao watakupa tiba au huduma za afya. Kwa mfano, ikiwa umefanyiwa upasuaji au umejifungua hivi karibuni, tunaweza kuwasiliana na shirika la huduma za afya nyumbani ili kupanga huduma za nyumbani au kuangalia kuhusu unavyoendelea baada ya kuondoka kwenye hospitali.

• **Kwa Malipo ya Huduma za Afya** Tunaweza kutumia na/au kufichua taarifa zako za afya ili kutoza na kupokea malipo kwa ajili ya huduma unazopata kutoka kwetu. Kwa mfano, tunaweza kutoa taarifa zako za afya kwa idara yetu ya bili au madai ili kutayarisha bili au taarifa ya kukutumia, kutumia kampuni yako ya bima, ikiwa ni pamoja na Medicare au Medicaid, au kundi au mtu mwingine anayelipia huduma zako za afya.

• **Kwa Shughuli Zetu za Huduma za Afya** Pia tunaweza kutumia au kutoa taarifa zako za afya ili kutekeleza shughuli fulani za usimamizi, kifedha, kisheria na uimarishaji ubora ambazo ni muhimu kwa ajili ya kuendesha biashara yetu na kusaidia kwa shughuli zetu za tiba na malipo. Kwa mfano, tunaweza kutumia na/au kufichua taarifa zako za afya ili kusaidia kutathmini ubora na utendaji wa madaktari na wafanyakazi wetu na kuboresha huduma tunazotoa. Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa madaktari, wataalamu wa matibabu, au watalaamu wengine wa afya au biashara kwa ajili ya ukaguzi, ushauri, ulinganishaji na mipango. Tunaweza kutumia na kufichua taarifa zako za afya wakati wa mipango ya mafunzo na shughuli za utambuaji rasmi, uthibitishaji, utoaji leseni na utoaji wa hati za utambulisho. Vilevile, tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa wakaguzi, wahasibu, wanasheria, wadhibiti wa serikali au washauri wengine ili kutathmini na/au kuhakikisha utii wa sheria au kutuwakilisha mbele ya mamlaka ya udhibiti au mamlaka mengine ya usimamizi au asasi za mahakama.

### Kwa Shughuli Zinazoruhisiwa au Zinazohitajika Kisheria

Kuna hali ambapo Health Insurance Portability and Accountability Act (Sheria ya Bima ya Afya ya Kuchukulika na Kuwajibika, HIPAA) huturuhusu kutumia na/au kufichua taarifa zako za afya bila kwanza kupata idhini yako ya maandishi kwa madhumuni mbali na tiba, malipo au shughuli nyingine za huduma za afya. Isipokuwa kwa hali mahususi ambapo sheria inatuhitaji kutumia na kufichua taarifa (kama vile ripoti za kuzaliwa kwenye idara ya afya au ripoti za dhuluma au utelekezaji wa huduma za jamii), tumeorodhesha matumizi na mifichuo yote inayoruhusiwa na HIPAA katika sehemu hii. Lazima tutimize masharti mengi katika sheria kabla hatujashiriki taarifa zako kwa madhumuni haya. Kwa maelezo zaidi, angalia hhs.gov/hipaa/for-individuals/guidance-materials-for-consumers/index.html.

**1. Shughuli za Afya ya Umma** Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa madhumuni ya afya ya umma, ikiwa ni pamoja na:

- kwa mamlaka ya afya ya umma ambayo yameidhinishwa kisheria kukusanya au kupokea taarifa ili kuripoti miongoni mwa mambo mengine, magonjwa ya kuambukiza na dhuluma kwa watoto
- kwa U.S. Food and Drug Administration (Shirika la Usimamizi wa Chakula na Dawa la Marekani, FDA) ili kuripoti kifaa cha matibabu au matukio yanayohusiana na bidhaa
- kuarifu mtu aliyeathiriwa na ugonjwa wa kuambukiza
- kwa mwajiri wako ikiwa tunatoa huduma kwa maelekezo ya mwajiri wako inayohusiana na jeraha la kazini
- kwa shule yako ikiwa thibitisho la chanjo limeombwa

**2. Kuripoti Uwezekano wa Dhuluma au Utelekezaji wa Mtu Mzima** Ikiwa tunaamini kwamba mgonjwa ni mwathiriwa wa dhuluma za nyumbani, tunaweza kuarifu shirika la serikali lililoidhinishwa kisheria kupokea ripoti za matatizo hayo. Katika hali nyingine, tunaweza kukuarifu kabla ya kuripoti masuala kama hayo.

**3. Shughuli za Usimamizi wa Huduma za Afya** Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa shirika la usimamizi wa huduma za afya lililoidhinishwa kisheria kufuatilia mfumo wa huduma za afya na utii wetu wa sheria fulani.

**4. Shughuli za Utekelezaji Sheria** Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kuhusiana na utekelezaji wa hati ya kuitwa mahakamani, amri ya kufika mahakamani, hati ya kufika mahakamani ya baraza la wazee wa mahakama, ombi la usimamizi, kibali, amri ya uchunguzi, au ombi la afisa wa utekelezaji sheria la taarifa za kutambua au kumtafuta mwathiriwa, mshukiwa, mkimbizi, mtu aliyepotea (pamoja na watu walioaga dunia), kuripoti uhalifu uliotekelezwa kwenye majengo yetu, au kuripoti uhalifu ambao huenda umesababisha haja ya huduma zetu za dharura. Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington kikipokea hati ya kuitwa mahakamani, amri ya kufika mahakamani, hati ya kufika mahakamani ya baraza la wazee wa mahakama, ombi la usimamizi, kibali, amri ya uchunguzi ambayo inahitaji Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington kisheria kufichua rekodi zako za afya, Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington kitajaribu kukupa notisi kabla ya kufichua taarifa zako za afya kwa mamlaka ya utekelezaji sheria ikiwa Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington kimeruhusiwa kufanya hivyo.

**5. Kesi za Mahakama na Utawala** Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kuhusiana na hati ya kufika mahakamani, amri ya mahakama au mahakama ya utawala, ombi la ugunduzi, au mchakato mwingine wa kisheria wakati wa kesi ya mahakama au utawala. Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington kitajaribu kukupa notisi kabla ya kufichua taarifa zako za afya isipokuwa notisi hiyo iwe imetolewa na mhusika mwingine kwenye mgogoro na/au amri ya ulinzi inayostahiki imewasilishwa katika mgogoro.

**6. Wachunguzi wa Vifo, Wachunguzi wa Matibabu na Wasimamizi wa Matanga** Tunaweza kufichua taarifa zak za afya kwa wachunguzi wa vifo, wachunguzi wa matibabu na wasimamizi wa matanga ili kutambua mtu aliyeaga dunia au kutambua chanzo cha kifo.

**7. Mchango wa Viungo** Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa shirika la kununua viungo au kituo kingine kinachoshiriki katika au kinachofanya uamuzi wa ununuzi, kuweka na/au upandikizaji wa viungo au tishu.

**8. Madhumuni ya Utafiti** Tunafanya na kushiriki katika utafiti wa matibabu, jamii, saikolojia na aina nyingine za utafiti. Miradi mingi inayomhusu binadamu, ikiwa ni pamoja na mingi ambayo inahusisha matumizi ya taarifa za afya, inazingatia mchakato wa idhini maalum inayotathmini mradi wa utafiti uliopendekezwa na matumizi yake ya taarifa za afya. Hata hivyo, katika hali fulani, tunaweza kufichua taarifa za afya kwa watafiti wanaojitayarisha kufanya mradi wa utafiti ili kuwasaidia kuamua ikiwa mradi wa utafiti unaweza kutekelezwa au iwapo utakuwa muhimu, mradi tu taarifa za afya wanazokagua haziondoki katika majengo yetu. Matabibu wetu wanaweza kukupa fursa ya kushiriki katika jaribio la utafiti wa kimatibabu (tiba za uchunguz) na watafiti wengine wanaweza kuwasiliana nawe kuhusu nia yako ya kushiriki katika miradi ya utafiti. Usajili wako katika mradi wa utafiti utatokea tu baada ya kufahamishwa kuhusu utafiti wenyewe, ya kupata fursa ya kuuliza maswali na kutia sahihi fomu ya ridhaa. Unapoidhinishwa kupitia mchakato maalum wa ukaguzi, utafiti unaweza kuendeshwa kwa kutumia taarifa zako za afya bila ridhaa yako.

**9. Kuepusha Madhara kwa Mtu au Usalama wa Umma** Tunaweza kufichua taarifa zako za afya ikiwa tunaamini kwamba ufichuaji ni muhimu ili kuzuia au kupunguza tisho au madhara mabaya kwa umma au afya au usalama wa mtu mwingine.

**10. Majukumu Maalum ya Serikali** Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa mahitaji mahususi ya usalama wa serikali, au inavyohitajika na asasi za urekebishaji.

**11. Madhumuni ya Fidia kwa Wafanyakazi** Tunaweza kufichua taarifa zako za afya ili kutii sheria za fidia kwa wafanyakazi au mipango kama hiyo.

**12. Kwa Washirika wa Kibiashara** Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa "washirika wetu wa kibiashara," ambao ni watu au kampuni zinazotupa huduma. Kwa mfano, mshirika wa kibiashara ni pamoja na kampuni inayosimamia madai ya bili kwa niaba yetu, muuzaji wa programu anayetusaidia kutuma vikumbusho kuhusu miadi na watoa huduma wengine. Tunahitaji washirika wa kibiashara walinde taarifa zako.

**13. Ili Kukufahamisha kuhusu Bidhaa au Huduma Zinazohusiana na Afya** Tunaweza kutumia au kufichua taarifa zako za afya kuwasiliana nawe kwa ajili ya miadi ya matibabu au huduma nyingine zilizoratibiwa, au kukupa taarifa kuhusu tiba mbadala au mafao na huduma zinazohusiana na afya.

**14. Kwa Wazazi na Walezi wa Kisheria wa Watoto Wachanga** Wakati mgonjwa ni mtoto mchanga ambaye hajakombolewa, tunaweza kushiriki taarifa za afya za mtoto mchanga na wazazi au walezi wa mgonjwa isipokuwa vinginevyo ipigwe marufuku na sheria.

**15. Madhumuni ya Bili na Ukusanyaji** Tunaweza kutumia au kufichua taarifa zako za afya kwa madhumuni ya kupata malipo kwa ajili ya huduma zilizotolewa. Tunaweza kuwasiliana nawe kwa njia ya barua au simu kwa mbari yoyote ya simu inayohusishwa nawe, ikiwa ni pamoja na nambari za pasiwaya. Simu zinaweza kupigwa kwa kutumia ujumbe wa sauti uliorekodiwa mapema au bandia na/au kifaa cha kupiga kiotomati ("autodialer"). Ujumbe unaweza kuachwa kwenye mashine au ujumbe wa sauti wa kujibu, ikiwa ni pamoja na taarifa yoyote ya ujumbe inayohitajika kisheria (ikiwa ni pamoja na sheria za ukusanyaji wa madeni) na/au kuhusu kiasi unachodaiwa. Ujumbe wa maandishi au barua pepe kwa kutumia anwani yoyote ya barua pepe unayotoa inaweza pia kutumiwa ili kuwasiliana nawe.

**16. Madhumuni ya Kuchangisha Pesa** Tunaweza kutumia au kufichua taarifa za demografia, ikiwa ni pamoja na majina, anwani, taarifa nyingine za mawasiliano, umri, jinsia na tarehe ya kuzaliwa; tarehe ambazo ulipokea huduma ya afya kutoka kwetu; idara ya taarifa za afya; taarifa ya daktari anayetibu; na taarifa ya matokeo ya kuwasiliana nawe ili kuchangisha fedha ili tuweze kuendelea au kupanua shughuli zetu za huduma za afya. Una haki ya kujiondoa kwenye mawasiliano haya ya uchangishaji fedha. Ikiwa usingependa tuwasiliane nawe kama sehemu ya jitihada za kuchangisha fedha, tafadhali wasiliana na watu walioorodheshwa hapa chini katika Sehemu ya Mawasiliano ya Notisi hii. Ukiamua kwamba hutaki tuwasiliane nawe kama sehemu ya jitihada za kuchangisha fedha, hatutaweka masharti kwenye huduma wala malipo baada ya uamuzi huo.

Tafadhali fahamu kwamba tukipokea taarifa zinazohusiiana na utambuzi wako wa ugonjwa, ubashiri wa ugonjwa, au tiba kwa tatizo la matumizi ya mihadarati kutoka kwa mshiriki wa mipango hadi 42 CFR Sehemu ya 2 ("Rekodi za Sehemu ya 2"), hatutatumia wala kufichua Rekodi zako za Sehemu ya 2, wala kutoa ushahidi unaoonyesha maudhui ya Rekodi zako za Sehemu ya 2, katika kesi yoyote ya kiraia, uhalifu, usimamizi, wala kisheria dhidi yako isipokuwa uwe umetoa ridhaa ya maandishi ya ufichuaji huu (tofauti na ridhaa yako kwa matumizi au ufichuaji mwingine wowote), au amri ya mahakama baada ya notisi na umepewa au tumepewa fursa ya kusikilizwa (kama mmiliki kisheria wa Rekodi ya Sehemu ya 2), kama ilivyotolewa na 42 CFR Sehemu ya 2. Amri ya mahakama inayoidhinisha matumizi au ufichuaji wa taarifa hizi lazima iandamane na hati ya kufika mahakamani au hitaji jingine la kisheria linaloshurutisha ufichuaji kabla ya taarifa zinazoombwa kutumiwa au kufichuliwa.

BJC Health huendesha mpango wa 42 CFR Part 2. Taarifa za ziada zinazohusiana na Notisi ya Desturi za Faragha ya mpango huu zinapatikana kwenye BJCBehavioralHealth.org.

## Wakati Mapendeleo Yako Yataongoza Matumizi au Ufichuaji Wetu

• Kitabu cha maelezo ya mawasiliano cha kituo kinaweza kujumuisha jina lako, mahali ulipo katika kituo, hali yako kwa jumla kama vile sawa, imara, nk., na imani yako ya kidini (ikiwa umetoa). Isipokuwa utuambie kwamba ungependa kuzuia taarifa zako katika kitabu cha maelezo ya mawasiliano ya kituo, utajumuishwa na taarifa za kitabu cha maelezo ya mawasiliano zinaweza kufichuliwa kwa viongozi wa kidini au kwa watu wanaokuulizia kwa jina.

• Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa mwanafamilia, jamaa mwingine, rafiki au mtu mwingine yeyote unayemtambua ambaye anahusika katika huduma yako au na malipo yanayohusiana na huduma yako isipokuwa utuambie
vinginevyo.

## Matumizi na Mifuchuo Inayohitaji Idhini Yako ya Maandishi

• Hatutafichua maelezo ya tiba ya saikolojia bila idhini yako ya maandishi isipokuwa matumizi na mfichuo uruhusiwe au kuhitajika vinginevyo na sheria.

• Hatutashiriki katika mifichuo inayohusu mauzo ya taarifa zako za afya bila idhini yako ya maandishi. Uuzaji wa taarifa za afya zinazolindwa hutokea wakati sisi au mtu mwingi tunayempa mkataba moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kupokea malipo kwa kubadilishana taarifa zako za afya zinazolindwa.

• Hatutatumia wala kufichua taarifa zako za afya zinazolindwa kwa madhumuni ya utafutaji soko bila idhini yako ya maandishi. Utafutaji soko unafafanuliwa kama upokeaji wa malipo kutoka kwa mtu mwingine kwa ajili ya kuwasiliana nawe kuhusu bidhaa au huduma iliyotolewa na mhusika mwingine.

Kwa hali ambazo hazijaelezwa kwa jumla katika Notisi hii, tutaomba idhini yako ya maandishi kabla hatujatumia wala kufichua taarifa zako za afya. Unaweza kubatilisha idhini hiyo, kwa maandishi, wakati wowote ili kuacha kufichua taarifa zako za afya siku zijazo. Hata hivyo, taarifa zilizofichuliwa awali hazitaombwa ili kurejeshwa wala ubatilishaji wako kuathiri hatua yoyote ambayo tayari tumechukua kulingana na idhini yako. Vilevile, ikiwa tulikusanya taarifa hizo kuhusiana na utafiti, tunaruhusiwa kutumia na kufichua taarifa hizo kwa muda unaohitajika ili kulinda hadhi ya utafiti.

## HAKI ZAKO KUHUSU TAARIFA ZAKO ZA AFYA

### Kuomba Vikwazo vya Matumizi na Mifichuo Fulani ya Taarifa za Afya

Unaweza kuomba vikwazo kuhusu jinsi tunavyotumia au kufichua taarifa zako za afya zinazolindwa kwa njia ya maandishi kwa ajili ya tiba, malipo kwa ajili ya huduma za afya tulizokupa, au shughuli zinazohusiana na huduma za afya. Pia unaweza kuomba vikwazo kuhusu taarifa za afya tunazoweza kufichua kwa mtu anayehusika katika huduma yako, kama vile mwanafamilia au rafiki. Ili kutuma ombi, tafadhali angalia maagizo yaliyo mwisho wa Notisi hii.

Hatuhitajiki kukubali ombi lako katika hali zote. Vilevile, kiwazo chochote tunachoweza kuidhinisha hakitaathiri matumizi wala ufichuaji wowote tunaohitajika au tunaoruhusiwa kufanya kwa mujibu wa sheria. Lazima tukubali ombi lako la vikwazo vya ufichuaji wa taarifa zako za afya kwa mpango wako wa afya ikiwa ufichuaji hauhitajiki kisheria na taarifa za afya unazotaka tuweke vikwazo zinahusiana na kipengee au huduma ya afya ambayo wewe (au mtu mwingine asiye mpango wako wa afya, kwa niaba yako) ulitulipa kikamilifu.

### Kuomba Mawasiliana ya Siri

Unaweza kuomba mabadiliko kwa njia ambayo tunawasiliana nawe au eneo ambalo tunawea kuwasiiana nawe. Lazima utume ombi lako kwa njia ya maandishi. Angalia taarifa za mawasiliano hapa chini. Tutakubali ombi lako linlofaa, lakini kuhusu kuamua ikiwa ombi lako linafaa, huenda tukazingatia ugumu wa usimamisi unaoweza kutuathiri.

### Kukagua na Kuchukua Nakala za Taarifa Zako za Afya

Unaweza kuangalia kwenye na/au kuchukua nakala ya taarifa zako za afya. Lazima utume ombi lako kwa njia ya maandishi. Ili kutuma ombi la taarifa zako za afya, tafadhali angalia maagizo yaliyo mwisho wa Notisi hii.

Huenda tukakutoza kwa ajili ya kunakili au kutayarisha muhtasari wa taarifa za afya ulizoomba. Tutajibu ombi lako la taarifa za afya ndani ya siku 30 baada ya kupokea ombi lako kwa kutoa taarifa ulizoomba, kukataa ombi kwa maelezo ya maandishi kuhusu kukataa, au kukushauri kwamba tunahitaji muda zaidi kukamilisha hatua yetu kuhusu ombi lako (kwa mfano, ikiwa taarifa zako za afya hazipatikani kwa sasa au taarifa zinahifadhiwa katika eneo la hifadhi lililo mbali na kituo).

### Kuomba Mabadiliko katika Taarifa Zako za Afya

Unaweza kuomba kwa njia ya maandishi, marekebisho au masahihisho ya taarifa zako za afya ikiwa unadhani kwamba taarifa zako za afya si sahihi au hazijakamilika. Hatuhitajiki kukubali ombi lako isipokuwa ikiwa inahitaji na sheria ya jimbo husika. Hakuna hali yoyote itakayotufanya tufute wala kuondoa hati zako halisi katika taarifa zako za afya isipokuwa iwe imeombwa kwa mujibu wa sheria za jimbo husika. Maagizo kuhusu jinsi ya kutuma ombi la marekebisho au masahihisho kwenye taarifa zako za afya yanaweza kupatikana nyuma ya Notisi hii.

### Kuomba Hesabu za Mifichuo ya Taarifa Zako za Afya

Unaweza kuomba kwa njia ya maandishi hesabu ya aina fulani za mifichuo ya taarifa zako za afya tuliyoifanya nmiaka sita kabla ya ombi lako. Sheria inaondoa kwenye hesabu mifichuo mingi ya kawaida, kama vile ile iliyofanywa ili kukuhudumia, kulipia huduma zako za afya, au pale ulipotoa idhini ya maandishi kwa ufichuaji.

Ili kutuma ombi la hesabu, angalia taarifa za mawasiliano hapa chini. Kwa jumla, tutajibu ombi lako ndani ya siku 60 baada ya kupokea ombi lako isipokuwa pale tutakapohitaji muda zaidi. Una haki ya hesabu moja kwa mwaka.

## MAJUKUMU YETU KUHUSU TAARIFA ZAKO ZA AFYA

### Arifa Kufuatia Ukiukaji wa Taarifa za Afya Zinazolindwa Zisizo na Ulinzi

Tunahitajika kisheria kukuarifu endapo taarifa zako za afya zinahusiana na ukiukaji tulioshuhudia ambao umeathiri faragha au usalama wa taarifa zako za afya.

### Kupata Notisi ya Desturi Zetu za Faragha

Tunahitajika kukupa Notisi yetu ii kueleza na kukufahamisha kuhusu Desturi zetu za Faragha. Hata ikiwa umeomba Notisi hii kielektroniki, unaweza kuomba nakala ya taarifa zako za ya karatasi wakati wowote. Pia unaweza kutazama au kupata nakala ya Notisi hii kwenye tovuti zetu: BJC.org/patients-visitors/patient-privacy, SaintLukesKC.org/patients-visitors/patient-privacy, and physicians.washu.edu/for-patients/for-your-protection/.

## MALALAMISHI

Tunakubali fursa ya kuangazia tatizo lolote unaloweza kuwa nalo kuhusu faragha ya taarifa zako za afya. Ikiwa unaamini kwamba faragha ya taarifa zako za afya imekiukwa, unaweza kuwasilisha malalamishi kwa watu walioorodheshwa katika Sehemu ya Mawasiliano ya Notisi hii. Pia unaweza kuwasilisha malalamishi kwa Secretary of the U.S. Department of Health and Human Services, Office for Civil Rights (Idara ya Huduma za Afya na Binadamu, Afisi ya Haki za Raia ya Marekani), kwa kutuma barua kwa 200 Independence Avenue, SW, Washington, DC 20201, kupiga simu 877-696-6775, au kutembelea hhs.gov/hipaa/filing-a-complaint/index.html.

Hatutalipiza kisasi dhidi yako kwa kuwailisha malalamishi kwetu au Afisi ya Haki za Raia.

*Kuanza Kufanya Kazi Tarehe: 16 Februari, 2026*

## TAARIFA ZA MAWASILIANO

Ni muhimu kufahamu kwamba maombi au malalamishi yako lazima yawasilishwe kwenye hospitali au afisi ambapo tatizo lako la faragha lilitokea. Ombi au lalamiko lolote kwa mtoa huduma mmoja halitasemekana kuwasilishwa kwa mtoa huduma yeyote anayefidiwa na au aliyetajwa katika Notisi hii ya Pamoja.

### Taarifa za Mawasiliano za Hospitali Shirika, Vituo na Watoa Huduma wa BJC Health:

• Kwa maswali kuhusu Notisi hii, kuripoti matatizo kuhusu Desturi zetu za Faragha, au kuwasilisha malalamishi kuhusu Desturi za Faragha za hospitali shirika na watoa huduma wa BJC Health, tafadhali wasiliana na Afisa wa Faragha kwa njia yoyote iliyoorodheshwa hapa chini:

**BJC Health — Afisa wa Faragha**
4901 Forest Park Ave., Suite 1140
Mailstop: 90-75-571
St. Louis, MO 63108
314-362-4855
Barua pepe: compliance@bjc.org

## Kwa BJC HealthCare:

• **Ili kuangalia au kupata nakala ya taarifa zako za afya** kutoka hospitlai shirika au mtoa huduma wa BJC HealthCare, unaweza kuwasiliana na 314-362-3935 au kutembelea BJC.org na kuwasiliana na idara ya rekodi za matibabu ya kituo amapo taarifa zako za afya zinahifadhiwa.

• **Ili kuomba marekebisho au masahihisho kwenye taarifa zako za afya** zinazohifadhiwa na hospitali shirika na watoa huduma wa BJC HealthCare, tafadhali tuma barua pepe enterprise_mpi_maintenance@bjc.org or call 314-273-2468.

• **Ili kuomba vikwazo kuhusu matumizi ya taarifa zako za afya** na hospitali shirika na watoa huduma wa BJC HealthCare, tafadhali tuma barua pepe kwa HIM_DMOPS_ROI@bjc.org.

• **Ili kuomba hesabu ya mifichu** na hospitali shirika na watoa huduma wa BJC HealthCare, tafadhali tuma barua pepe kwa disclosure_management_legal@bjc.org or call 314-454-4997.

## Kwa Saint Luke’s:

• **Ili kuangalia au kuchukua nakala ya taarifa zako za afya** kutoka hospitali au mtoa huduma wa Saint Luke’, unaweza kuwasiliana na idara ya Rekodi za Matibabu/Utoaji wa Taarifa kwa barua pepe kwenye roi@saint-lukes.org, au tembelea saintlukeskc.org/medical-records.

• **Ili kuomba marekebisho au masahihisho kwneye taarifa zako za afya** zinazohifadhiwa na hospitali shirika na watoa huduma, tafadhali jaza na uwasilishe fomu inayopatikana kwenye saintlukeskc.org/medical-records na uwasilishe kupitia barua pepe kwa amendments@saintlukeskc.org.

• **Ili kuomba vikwazo kwenye matumizii ya taarifa zako za afya** na hospitali shirika na watoa huduma wa Saint Luke’s, tafadhali wasiliana na Rekodi za Matibabu kwenye roi@saint-lukes.org.

• **Ili kuomba hesabu ya mifichuo** na hospitali shirika na watoa huduma wa Saint Luke’s, tafadhali wasiliana na Rekodi za Matibabu kwenye roi@saint-lukes.org.

## Taarifa za Mawasiliano ya Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington au Watoa Huduma wake:

• Kwa maswali kuhusu Notisi hii, matatizo kuhusu Desturi zetu za Faragha, au kuwasilisha malalamishi kuhusu Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington au watoa huduma wake, unaweza kuwasiliana na Afisa wa Faragha kwa njia yoyote kati ya zilizoorodheshwa hapa chini:

**Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington — Afisa wa Faragha**
660 S. Euclid Ave.
MSC 8095-02-01
St. Louis, MO 63110
866-747-4975
Barua pepe: HIPAA@wustl.edu

• **Ili kuangalia au kupata nakala ya taarifa zako za afya** kutoka kwa mtoa huduma wake wa Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington, tafadhali fuata maelekezo yanayopatikana kwenye physicians.washu.edu/for-patients/medical-records-request/. Pia unaweza kuwasiliana na Washington University Health Information Release Service kwa 314-273-0453.

• **Ili kuomba marekebisho au masahihisho** kwenye taarifa zako za afya na mtoa huduma wa Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington, tafadhali fuata maelekezo yanayopatikana kwenye physicians.washu.edu/for-patients/medical-records-request/ au wasiliana na Usimamzi wa Taarifa za Matibabu wa Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington kwa barua pepe kwenye HIM@wustl.edu au kwa simu nambari 314-273-1986.

• **Ili kuomba vikwazo kwneye matumizi ya taarifa zako za afya** na mtoa huduma wa Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington, tafadhali wasiliana na Afisi ya Faragha ya HIPAA ya Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington kwa nambari 866-747-4975 au kwa barua pepe kwenye HIPAA@wustl.edu.

• **Ili kuomba hesabu ya mifichuo** na mtoa huduma wa Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington, tafadhali wasiliana na Afisi ya Faragha ya HIPAA ya Chuko Kikuu cha Matibabu cha Washington kwa nambari 866-747-4975 au barua pepe kwenye HIPAA@wustl.edu.

MASHIRIKA YANAYOTII NOTISI HII YANAPATIKANA KWENYE KIUNGO KIFUATACHO:

BJC.org/patients-visitors/patient-privacy